



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO
BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)



ONYO

ONYO KWA WASANII WANAOSAMBAZA PICHA NA VIDEO KINYUME NA MAADILI.

18 Septemba, 2023.

Baraza la Sanaa la Taifa kupitia Sheria Na. 23 ya Mwaka 1984 na Marekebisho yake ya Mwaka 2019 inatoa Mamlaka kwa Baraza la Sanaa la Taifa kusimamia Maadili ya msingi kwenye Sekta ya Sanaa pamoja na kukuza na kuendeleza Sanaa kwa **Kanuni ya 25(1)-(8)** ya Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa za Mwaka 2018.

Hivi karibuni kumetokea wimbi la Wasanii kuwa na tabia ya kupiga picha, kujirekodi au ku-rekodiwa video zenye maudhui kinyume na maadili ya Kitanzania kisha kusambaza kwenye mitandao ya kijamii kinyume na Sheria na kanuni za uendeshaji wa shughuli za Sanaa nchini.

Hivyo basi, Baraza linatoa onyo Kali Kwa wasanii wote kuacha tabia ya kujirekodi au ku-rekodiwa na kusambaza picha au video zisizo na Maadili kwenye mitandao ya kijamii kwani kufanya hivyo ni kinyume cha Sheria na kanuni za uendeshaji wa shughuli za Sanaa na Maadili ya Kitanzania.

Baraza halitasita kuchukua hatua Kali ikiwemo kufutiwa leseni na Kibali cha kujishughulisha na kazi ya Sanaa kwa wote watakaoenda kinyume na tamko hili kwani itatafsiriwa kuwa ni uvunjaji wa sheria.

Imetolewa na,

Isack N. Bilali,

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,

Baraza la Sanaa la Taifa-BASATA

Jengo la Utumishi Block B/C/D, 8 Barabara ya Kivukoni, S. L. P 4779, Ilala, Dar es Salaam Simu:
255 22 2863748 Barua pepe: info@basata.go.tz Tovuti: www.basata.go.tz